# FAHAMU HAKI ZAKO

Kijitabu cha habari kinachoelezea haki zako wakati unapofanya kazi nchini Marekani.

Nambari Maalum ya Kitaifa Dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu
**1-888-373-7888** (ndani ya Marekani)











# FAHAMU HAKI ZAKO

Tuna hakika kwamba utafaidika na kukaa kwako nchini Marekani. Hata hivyo, endapo matatizo yakitokea unazo haki na unaweza kupata msaada!

### Unayo Haki ya:

- Kulipwa malipo stahiki
- Kuwa huru kutokana na ubaguzi
- Kuwa huru kutokana na unyanyasaji wa kijinsia na unyonyaji wa kingono
- Kuwa na mahali pa kazi penye afya na salama
- Kuomba msaada kutoka kwa vyama vya wafanyakazi, makundi ya wahamiaji, na yanayotetea haki za wafanyakazi
- Kuondoka kwenye ajira yenye mazingira ya uonevu

**UKIONEWA, WASILIANA NA NAMBARI MAALUM YA KITAIFA DHIDI YA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU AMBAYO NI 1-888-373-7888 (NDANI YA MAREKANI), TUMA UJUMBE MFUPI WA "SAIDIA" KWA 233733 (NDANI YA MAREKANI) AU TUMA BARUA PEPE KWA *NHTRC@POLARISPROJECT.ORG.***

**WATAALAMU WENYE MAFUNZO DAIMA WANAPATIKANA KUSAIDIA KATIKA LUGHA ZAIDI YA 200. SI LAZIMA UTOE JINA LAKO AU KUJITAMBULISHA. JIFUNZE MENGI ZAIDI KWENYE TOVUTI YA *WWW.TRAFFICKINGRESOURCECENTER.ORG.***

Kama uko katika dharura ya hatari, ita polisi kwenye namba 911 (ndani ya Marekani). Waeleze dharura uliyonayo, taja eneo lako na namba ya simu ambayo unatumia kuita. Omba upewe mkalimani kama hujui Kiingereza. Polisi wakifika, unaweza kuwaonyesha kijitabu hiki na kuwaambia kuhusu uonevu uliokupata.

Ukipata viza aina ya A-3, G-5, H, J, NATO-7, au B-1 ya mfanyakazi wa nyumbani asiye mhamiaji, unapaswa kupokea kijitabu hiki wakati wa mahojiano yako ya viza. Lazima afisa wa konsula athibitishe kwamba umepokea, kusoma, na kuelewa yaliyomo ndani ya kijitabu hiki kabla hujapokea viza. Kama hujafanya hivyo, afisa wa konsula anapaswa kukupa kijitabu hiki na kujadiliana nawe masuala yaliyomo. Aidha, afisa wa konsula anapaswa kujibu maswali yoyote uliyo nayo kuhusu habari zilizomo katika kijitabu hiki.



# HAKI ZAKO BILA KUJALI HADHI YA VIZA

Kama unaamini kwamba haki zako zimekiukwa, toa ripoti ya hali hiyo kwa taasisi ya serikali, chama cha wafanyakazi, shirika lisilo la kiserikali, au shirika jingine linaloweza kukusaidia. Kama hujui Kiingereza, omba upewe mkalimani.

### 1. Haki yako ya Kulipwa Malipo Stahiki

- Una haki ya kulipwa kwa kazi yote unayofanya.
- Una haki ya kupata angalau mshahara wa kima cha chini kisheria wa serikali kuu kwa kazi zilizo nyingi. Tazama *www.dol.gov/whd/minimumwage.htm* kwa kima cha chini cha serikali kuu kwa sasa.
- Unaweza kuwa na haki ya kulipwa zaidi ya kima cha chini cha serikali kuu kama:
  - Unafanya kazi katika jimbo, mji, au kaunti ambayo ina mshahara wa juu wa kima cha chini.
  - Mkataba wako wa ajira/programu ya viza inahitaji kiwango cha juu.
- Unaweza ukawa na haki ya kulipwa ovataimu ya mara moja na nusu ya kiwango cha mshahara wako wa kila saa kwa masaa yoyote uliyofanya kazi nyongeza zaidi ya masaa 40 kwa wiki. Kwa mfano, kama mshahara wako wa kawaida ni $10 kwa saa, huenda mwajiri wako akatakiwa kukulipa $15 kwa kila saa unayofanya kazi zaidi ya masaa 40 katika muda wa wiki moja.
- Kama mwajiri wako anachukua pesa kutoka kwenye malipo yako, hili linaitwa kato. Lazima mwajiri wako akufahamishe kwa uwazi kila kato linalochukuliwa kutoka kwenye malipo yako.
- Makato huenda yakawa kinyume cha sheria ikiwa unabakia na chini ya kima cha mshahara kinachohitajika kisheria baada ya makato. Kwa kawaida mwajiri huenda asikate malipo kwa gharama za sare, vifaa vya usalama, vitendea kazi vinavyohitajika, mahitaji, vifaa au ada za uandikishaji. Kwa baadhi ya aina za viza, makazi lazima yatolewe bure bila malipo.

**DOKEZO: Leta kijitabu hiki utakapokuja Marekani ili kiwe kumbukumbu mnamo siku za baadaye.**



DOKEZO: Kulingana na urefu wa muda wako wa kukaa, unaweza kutakiwa kuwa na bima ya afya ukiwa nchini Marekani. Unaweza pia kustahili kupata msaada wa kifedha ili kupunguza gharama ya bima ya afya.

- Makato halali yanajumuisha yale unayoyachagua, kama vile bima ya afya, ada za chama cha wafanyakazi, au mkopo wa mshahara, na vile vile makato ambayo mwajiri lazima ayafanye kutokana na mazuio yaliyoamuriwa na mahakama kwa ajili ya msaada wa watoto au masurufu, au utaratibu wa muflisi. Kwa kiasi kikubwa, watu wenye viza zisizo za wahamiaji na wanaofanya kazi nchini Marekani wanalazimika kulipa kodi za mapato na ajira za serikali kuu na majimbo.Wewe pamoja na mwajiri wako mnaweza kukubaliana ili kodi ya mapato izuiliwe moja kwa moja kutoka kwenye malipo yako. Mwajiri wako kwa kawaida atazuia kodi za ajira, ikiwa ni pamoja na kodi ya Mfuko wa Hifadhi ya Kijamii na Mpango wa Serikali wa Bima ya Afya, moja kwa moja kutoka kwenye malipo yako.

### 2. Haki yako ya Kuwa Huru kutokana na Ubaguzi

- Ni kinyume cha sheria kwa mwajiri wako kukutendea wewe tofauti au vibaya kazini kwa sababu ya umri wako (kama wewe una miaka 40 au zaidi), jinsia au jinsi, jadi, asili ya utaifa na kabila, rangi, dini, habari za kijenetiki (ikiwa ni pamoja na historia ya matibabu ya familia), au ulemavu.
- Mwajiri wako hapaswi kukutendea tofauti kwa sababu wewe ni mwanamke au kwa sababu wewe ni mjamzito, unanyonyesha mtoto, au huenda ukapata mimba.

### 3. Haki Zako za Kuwa Huru kutokana na Unyanyasaji wa Kijinsia na Unyonyaji wa Kimapenzi

- Ni kinyume cha sheria kwa mwajiri wako kukunyanyasa kingono. Mwajiri wako hapaswi kutoa matamshi yoyote yanayochukiza kingono au kijinsia.



DOKEZO: Kabla ya kusafiri kwenda Marekani, pata ushauri kutoka kwa mashirika ya wafanyakazi wahamaji au wafanyakazi wahamaji wa zamani. Wanaweza kukupa majina na nambari za watu au mashirika unayoweza kuwasiliana nayo kama una matatizo au maswali utakapokuwa nchini Marekani.



- Ni kinyume cha sheria kwa mwajiri wako kukunyonya kingono, ikiwa ni pamoja na:
- Kudai kwamba ufanye kitendo chochote cha kujamiana;
- Kukugusa kwa njia ya kingono;
- Kukulazimisha, kukudanganya au kukushurutisha ufanye kitendo chochote cha kujamiana.

### 4. Haki yako ya kuwa Mahali Penye Afya na Usalama Kazini

Kama mfanyakazi nchini Marekani, una haki ya kuwa katika mazingira ya kazi yenye afya na salama, ikiwa ni pamoja na:

- **Matibabu:** Una haki ya kuripoti majeraha na magonjwa ya kazini kwa mwajiri wako. Ukijeruhiwa au kuugua kazini, unaweza kutafuta matibabu. Mara nyingi, kwa majeraha au magonjwa ya kazini, mwajiri wako anapaswa kutoa matibabu ya bure na sehemu ya mshahara ulioukosa wakati ulipokuwa umejeruhiwa. Huenda itakubidi uandikishe madai rasmi ya fidia ya wafanyakazi katika jimbo unakofanyia kazi.
- **Vifaa vya kinga:** Ukifanya kazi na au karibu na viuadudu au kemikali hatari, lazima mwajiri wako alipie na kutoa vifaa vya kinga vinavyohitajika kazini (kama vile kipumulio au glovu).
- **Mafunzo:** Una haki ya kupata habari na mafunzo kuhusu hatari, mbinu za kuzuia madhara, na usalama na viwango vya afya vinavyotumika kazini kwako. Lazima mafunzo yawe katika lugha na msamiati unaoweza kuelewa.
- **Makazi:** Kama mwajiri wako hutoa makazi, yanapaswa yawe safi na salama. Lazima uruhusiwe kuondoka kwenye makazi yako wakati wa saa zisizo za kazi.



- **Mabafu:** Lazima vyoo viwe safi na sehemu inayofikika kwa urahisi. Mwajiri wako anapaswa akupe nafasi ya kutumia vifaa vya chooni kama inavyohitajika.
- **Maji yanayonyweka:** Una haki ya kupata maji safi ya kunywa.
- **Sabuni na Maji Safi:** Una haki ya kunawa mikono yako kama inavyohitajika kwa sabuni na maji hasa baada ya kushika viuadudu/kemikali, ikiwa ni pamoja na mboga au matunda yaliyohifadhiwa kwa kunyunyiziwa viuadudu/kemikali.
- **Dharura za Kimatibabu:** Huenda gharama zako zikalipwa, hivyo unapaswa kumwambia mwajiri wako kuhusu jeraha lako au ugonjwa wako haraka iwezekanavyo ili mwajiri aweze kuwasilisha nyaraka muhimu. Ukiwa kwa daktari, kwenye zahanati, au hospitali, omba nakala za nyaraka kuhusu ugonjwa wako au jeraha lako.

Kama unafanya kazi na au karibu na viuadudu au kemikali hatari:

- Una haki ya kujua na kuelewa kemikali unazofanya kazi nazo, na mwajiri wako lazima akupe mafunzo yasiyoathiri mshahara wako kuhusu kemikali za kazini.
- Mwajiri wako lazima akuambie ni wapi na lini viuadudu vilinyunyiziwa na wakati ambao ni salama tena kuingia eneo lililowekwa dawa ili kuepuka kuhatarishwa kimakosa. Usiwe katika eneo ambapo viuadudu vinatumika.

### 5. Haki yako ya Kuomba Msaada kutoka Chama cha Wafanyakazi, Makundi ya Wahamiaji, na yale ya Haki za Wafanyakazi

- Kwa kiasi kikubwa, una haki ya kujiunga pamoja na wafanyakazi wenzako ili kumwomba mwajiri wako kuboresha mshahara wako au mazingira ya kazi. Wafanyakazi walio wengi pia wana haki ya kuanzisha, kujiunga, na kuunga mkono chama cha wafanyakazi mahali pako pa kazi.

DOKEZO: Ushauri wa kisheria kutoka kwa mwajiri, mkandarasi, au mtu aliyekutafutia kazi huenda ukawa na upendeleo. Tafuta ushauri kutoka kwa wakili wa kujitegemea.



- Wakati ambapo hufanyi kazi, unaweza kuhudhuria mikutano ya hadhara, mikusanyiko na maandamano ya kuunga mkono mishahara ya juu au mazingira bora ya kufanyia kazi mahali unapofanya kazi.
- Una haki hii bila ya kujali hadhi yako ya uhamiaji. Mwajiri wako hawezi kukuchukulia hatua kwa kudai haki zako.

### 6. Haki Yako ya Kuacha Ajira yenye Hali ya Uonevu

- Kitu kilicho muhimu zaidi ni kwako wewe kutafuta usalama kama unaonewa. Si lazima uendelee kukaa kwenye ajira yako kama mwajiri wako anakuonea.
- Ingawa hadhi yako ya viza haitakuwa halali tena ukimwacha mwajiri wako, huenda utaweza kubadilisha hadhi yako ya viza au mwajiri wako. Inawezekana utahitajika kuondoka Marekani ili kufanya hivyo. Hata kama hadhi ya viza yako si halali, msaada unapatikana punde unapomwacha mwajiri muonevu.
- Unaweza kufungua malalamiko rasmi au kuandikisha madai mahakamani dhidi ya mwajiri wako wakati unapofanya kazi au baada ya kumwacha mwajiri wako. Mwajiri wako akikuchukulia hatua (au kulipiza kisasi) kwa kufanya hivyo, anakiuka sheria.

## HAKI ZA ZIADA KULINGANA NA HADHI YAKO ISIYO YA UHAMIAJI

### Wafanyakazi wa Nyumbani wenye A-3, G-5, NATO-7, na B-1

- Mwajiri wako lazima akupe mkataba wa ajira unaofuata sheria za Marekani.
- Mkataba lazima utaje mshahara wa saa anaolipwa mfanyakazi wa nyumbani. Mshahara wa saa lazima uwe ambao ni mkubwa zaidi kati ya viwango vya mshahara wa kima cha chini kulingana na sheria za Serikali Kuu ya Marekani, majimbo, au serikali za mitaa.
- Waajiri lazima wakupe mkataba katika lugha unayoelewa. Hakikisha kwamba unaelewa masharti ya mkataba na usisaini hati yeyote kama hujui inasema nini.

### Mahitaji ya ziada kwa Wafanyakazi wa Majumbani wenye A-3, G-5, na NATO-7

*Angalau, lazima mkataba ujumuishe masharti yafuatayo:*

- Makubaliano ya mwajiri wako ya kutii sheria zote nchini Marekani;
- Taarifa kuhusu mzunguko na muundo wa malipo, wajibu kazini, masaa ya kazi kwa wiki, sikukuu, siku za ugonjwa, na siku za likizo; na

- Makubaliano ya mwajiri wako kutozuilia pasipoti yako, mkataba wa ajira, au mali zako nyingine binafsi.

### Viza za H-2A za Muda za Wafanyakazi wa Kilimo

- Hulazimiki kamwe kulipa ada kwa mtu anayekutafutia ajira.
- Lazima upokee mkataba wa kazi ulioandikwa katika lugha unayoelewa. Mkataba huo lazima uwe na taarifa za kina kuhusu mshahara, muda wa kazi, masaa, mafao (ikiwa ni pamoja na usafirishaji, makazi na milo au vifaa vya kupikia), na makato yoyote kutoka kwenye malipo yako.
- Una haki ya kulipwa kwa uhaki hata kama unalipwa kwa kima cha kipande.
- Mwajiri wako lazima ama akupatie au kukulipia gharama za usafiri wa kuingia nchini na masurufu kutoka mahali ambapo umetokea ili kuja Marekani kumfanyia kazi mwajiri hadi mahali pa ajira, au kukufidia kwa gharama stahiki mara unapokamilisha nusu ya mkataba wako wa kazi. Mara unapokamilisha mkataba wa kazi, mwajiri wako lazima akupe au akulipie gharama za usafiri wa kukurudisha pamoja na masurufu kutoka kituo cha kazi hadi mahali ulipotokea ili kuja kumfanyia kazi mwajiri. Mwajiri wako huenda akatakiwa kukufidia gharama zako za usafiri wa kuingia nchini na zile za viza katika wiki ya kwanza ya kazi endapo mshahara wako bila gharama zako ni mdogo kuliko mshahara wa kima cha chini cha Marekani. Mwajiri wako pia lazima akupe usafiri wa bure kutoka kwenye makazi yako yaliyotolewa na mwajiri kwenda sehemu ya kazi.
- Una msamaha wa kutolipa kodi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na zile za Mpango wa Serikali wa Bima ya Afya kutoka kwenye malipo uliyolipwa kwa huduma ulizotenda kuhusiana na viza yako ya H-2A.
- Kwa kawaida, mwajiri wako lazima akupe ajira yenye jumla ya masaa sawa na angalau ¾ ya siku za kazi katika kipindi cha mkataba.

### Viza za H-2B za Muda za Wafanyakazi Wasio wa Kilimo

- Hulazimiki kamwe kulipa ada kwa mtu anayekutafutia ajira.
- Lazima upokee barua ya ajira iliyoandikwa kwa lugha unayoelewa. Lazima barua hiyo iwe na taarifa za kina kuhusu mshahara, muda wa kazi, masaa, faida (ikiwa ni pamoja na usafirishaji, makazi na milo au vifaa vya kupikia), na makato yoyote kutoka kwenye malipo yako.
- Kwa kawaida, mwajiri wako lazima akupe ajira yenye jumla ya masaa sawa na angalau ¾ za siku za kazi katika kila kipindi cha wiki 12.
- Una haki ya kulipwa kwa uhaki hata kama unalipwa kwa kima cha kipande.





DOKEZO: Mwajiri wako lazima akulipe kwa wakati. Ni jambo la kawaida nchini Marekani kwa wafanyakazi kulipwa mara moja kila baada ya wiki mbili.

- Mwajiri wako lazima ama akupe au afidie gharama za ufasiri wa kuingia nchini pamoja na masurufu kutoka ng'ambo wakati utakapokuwa umekamilisha nusu ya kipindi cha mkataba. Aidha, mwajiri wako lazima alipe gharama za usafiri wako kwenda nyumbani, ikiwa ni pamoja na masurufu, endapo utakamilisha kipindi cha ajira au ukifukuzwa kazini na mwajiri wako kwa sababu yoyote kabla ya mwisho wa kipindi chako cha ajira kilichoidhinishwa. Mwajiri wako pia huenda akatakiwa kukufidia gharama zako za usafiri wa kuingia nchini na zile za viza mnamo wiki ya kwanza ya kazi endapo mshahara wako bila gharama zako ni mdogo kuliko mshahara wa kima cha chini cha Marekani.

### Viza za J-1 za Wageni wa Mabadilishano

- DS-2019 yako iliyoidhinishwa inaelezea tarehe za programu yako, aina ya mabadilishano, jina la mdhamini wako, na taasisi mwenyeji ambapo programu yako ya mabadilishano itafanyika.
- Mdhamini wako lazima aeleze kwa usahihi gharama, masharti, na vizuizi vyote katika programu yako ya mabadilishano.

### Kusafiri kwa Kazi Majira ya Joto

- Kama huna ajira iliyobainishwa awali, mdhamini wako lazima akusaidie kutafuta ajira mara utakapofika Marekani.

### Mfanyakazi Mwanafunzi au Mkurufunzi

- Mdhamini wako lazima akuhoji binafsi, kwa njia ya simu, au kwa kamera za mtandao.
- Mdhamini wako lazima akupe mpango wa ajira ya mfanyakazi mwanafunzi au mkurufunzi (DS-7002) ambao unajumuisha taarifa



ya maandishi ya mapato yoyote utakayopokea na muhtasari wa malengo ya mafunzo ya programu. Lazima upewe angalau masaa 32 ya kazi kwa wiki.

- Mdhamini wako lazima akupe taarifa ya maandishi ya gharama na ada utakazolazimika kulipa na pia makadirio ya gharama za maisha nchini Marekani.
- Mdhamini wako lazima ahakikishe kwamba una bima ya matibabu, ingawa mdhamini wako hahitajiki kutoa au kulipia bima hii.

### Mtumishi wa Nyumbani wa Kigeni:

- Familia yako mwenyeji lazima ikusaidie kujiandikisha na kuhudhuria madarasa katika taasisi ya masomo ya kiwango cha zaidi ya sekondari na kulipa hadi $500 kwa gharama za madarasa hayo.
- Wewe huhitajiki kufanya kazi kwa zaidi ya masaa 10 kwa siku au masaa 45 kwa wiki.
- Mshauri wako lazima adumishe mawasiliano ya mara kwa mara nawe pamoja na familia yako mwenyeji.

DOKEZO: Kabla ya kusafiri, tengeneza nakala mbili za nyaraka zote muhimu, hasa pasipoti yako na viza yako ya Marekani, mkataba wako wa ajira, na nyaraka zozote za ziada za utambulisho. Mpe seti moja ya nakala hizi mtu yeyote unayemwamini nchini mwako, halafu na wewe chukua seti nyingine uwe nayo.






# VIZA YAKO ISIYO YA MHAMIAJI

Viza isiyo ya mhamiaji ni hati ya serikali ya Marekani inayowaruhusu watu ambao wanasafiri kwenda Marekani kuomba kuingia huko kwa lengo fulani, ikiwa ni pamoja na kufanya kazi, kusoma, au kushiriki programu ya mabadilishano ya kiutamaduni. Lazima upate viza isiyo ya mhamiaji kwenye ubalozi au ofisi ya ubalozi mdogo wa Marekani ulioko nchi za nje. Mara baada ya kupata viza isiyo ya mhamiaji, unaweza kusafiri hadi Marekani na kuionyesha kwa ofisa wa uhamiaji wa Marekani kwa ajili ya kupata ruhusa ya kuingia nchini. Muda wa viza yako ukiisha, unahitaji kupata viza mpya kabla ya kuingia Marekani tena.

Unaporuhusiwa kuingia Marekani, ofisa wa uhamiaji ataigonga muhuri pasipoti yako na kuiweka alama ya tarehe ya ruhusa ya kuingia, daraja la ruhusa ya kuingia na tarehe ya "ruhusu kuingia hadi." Unahitaji kuondoka



Marekani kabla ya tarehe yako ya I-94 ya "ruhusu kuingia hadi"ili ubaki katika hadhi ya kisheria isipokuwa ukitoa maombi rasmi ya nyongeza kwenye Idara ya Marekani ya Huduma za Uraia na Uhamiaji. Unaweza kuangalia rekodi zako za I-94 kwenye *https://i94.cbp.dhs.gov*.



DOKEZO: Mara baada ya kuwasili nchini Marekani, weka pasipoti yako na nyaraka nyingine za kusafiri katika mahali salama ambapo unaweza kuzipata wakati wowote. Ni kinyume cha sheria kwa mwajiri wako kuchukua pasipoti yako.

# USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

Wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu wana haki ya ulinzi na huduma, na huenda wakastahili mafao fulani ya umma. Usafirishaji haramu wa binadamu ni uhalifu unaohusisha unyonyaji wa watoto kwa ajili ya biashara ya ngono, wa watu wazima kwenye biashara ya ngono kwa njia ya kulazimishwa, udanganyifu, au masharti, na wa mtu yeyote kwa kazi ya kulazimishwa. Watu wanaojihusisha na unyonyaji kama huo, wanaoweza kujumuisha wasafirishaji haramu wa wafanyakazi, makuwadi na wanunuzi wa biashara ya ngono, wanaweza kushtakiwa chini ya sheria za serikali kuu na majimbo dhidi ya biashara haramu. Wasafirishaji haramu wa wafanyakazi na wasafirishaji haramu wa biashara ya ngono wanaweza kushtakiwa kwa kosa la jinai na vilevile kukabiliwa na mashtaka ya kiraia. Zifuatazo ni baadhi ya ishara za onyo zinazoweza kuashiria usafirishaji haramu wa binadamu.

## Vitisho na Hofu

Wafanyabiashara haramu, na watu wanaowasaidia, huenda wakatumia vitisho na vitendo vingine vinavyoogofya ili kukufanya wewe au watu wengine kuhisi hofu kiasi cha kuogopa kujaribu kuondoka. Kwa mfano:

- Vipigo, uonevu wa kimwili, au uonevu wa kingono;
- Vitisho vya vipigo, uonevu wa kimwili, au uonevu wa kingono;
- Kumfungia mfanyakazi ndani au kumzuia asiondoke kazini au nyumbani;
- Vitisho vya kukudhuru wewe au familia yako ukijaribu kuondoka, kulalamikia maonevu, kuripoti hali hiyo kwa mamlaka, au kutafuta msaada;
- Vitisho kwamba unaweza kufukuzwa nchini au kukamatwa kwa sababu ya kutafuta msaada; au
- Vitisho au madhara yanayowakabili wafanyakazi wengine ambao wamejaribu kuondoka, kulalamika, kuripoti hali hiyo au kutafuta msaada, au vitisho kwamba mtu yeyote atakayejaribu kutoroka atapatikana na kurudishwa.

## Deni

Wafanyabiashara haramu, na watu wanaowasaidia, huenda wakadai kwamba wewe ufanye kazi, huduma au vitendo vya biashara ya ngono (ukahaba) ili ulipe deni. Mara nyingine deni linatengenezwa na kutozwa na mfanyabiashara haramu. Ni kinyume cha sheria kutumia deni kukulazimisha wewe kuendelea kufanya kazi, kutoa huduma au vitendo vya biashara ya ngono, au kukuzuia usiondoke. Wafanyabiashara haramu huenda wakafanya ulaghai wa hila na deni lako ili kulifanya liwe vigumu kulilipa na huenda wakakusababisha wewe kuamini kwamba lazima ubaki katika huduma ya mfanyabiashara haramu mpaka deni lilipwe. Mifano ya ulaghai wa hila wa madeni ni pamoja na:

- Kutoza deni ambalo ni vigumu au haiwezekani kulilipa kwa muda muafaka na ambalo liko nje ya uwiano wa kile utakacholipwa;
- Kutoza deni ambalo wewe hukukubaliana nalo mapema au ni kubwa kuliko deni ulilolikubalia;
- Kukataa kutumia mapato yako kwa malipo ya madeni;
- Kukataa kufafanua ni muda gani wewe utalazimika kukaa katika huduma ya mfanyabiashara haramu ili kulipa deni hilo;
- Kuongeza ada za usafirishaji, makazi, chakula, na malipo ya deni ambayo wewe hukuyakubalia tangu mapema; na
- Kuongeza malipo, faini au adhabu za kuvunja sheria, za kutoingiza kipato cha kutosha, au za kutofanya kazi, huduma au vitendo vya biashara ya ngono vya kutosha.

## Kanuni na Udhibiti

Wafanyabiashara haramu, na watu wanaowasaidia, huenda wakatumia kanuni na udhibiti ili kutatiza uwezo wako na ule wa watu wengine kuondoka, kulalamika, au kutafuta msaada. Kwa mfano:

- Masharti dhidi ya kuondoka mahali pa kazi, au masharti magumu kuhusu mahali unapoweza kwenda wakati ambapo hufanyi kazi;

DOKEZO: Weka rekodi ya kina ya kauli yoyote isiyofaa na/au hatua ambayo mwajiri wako anakuchukulia na uandike majina na namba za simu za mashahidi wowote.

- Masharti dhidi ya kuweka pasipoti yako mwenyewe, viza, cheti cha kuzaliwa, au nyaraka nyingine za utambulisho;
- Kunyimwa huduma ya kupata chakula, usingizi, au huduma za matibabu za kutosha; au
- Kuzuia, kudhibiti au kufuatilia mawasiliano yako na familia yako, wafanyakazi wengine, wateja, au watu wengine waliopo nje ya mahali pa kazi, kama vile wafanyakazi wa asasi za utoaji huduma za kisheria au kijamii.

### Udanganyifu na Uongo

Wafanyabiashara haramu, na watu wanaowasaidia, huenda wakatumia udanganyifu na uongo. Kwa mfano:

- Ahadi za uongo kuhusu aina ya kazi, masaa ya kufanya kazi, mazingira ya kazi au hali ya maisha, au malipo;
- Kukuahidi kazi nzuri halafu kukuhitaji ufanye kazi kwa masaa marefu mno, katika mazingira magumu, au kwa malipo madogo zaidi kuliko yaliyoahidiwa; au
- Kukuahidi kazi nzuri halafu kukulazimisha ufanye aina nyingine ya kazi, huduma, au vitendo vya biashara ya ngono; hivi vinaweza kujumuisha kukuahidi kazi kama profesa wa uuguzi, halafu kukulazimisha ufanye kazi kama mfanyakazi katika nyumba ya kutunza wazee, au kukuahidi kazi kama yaya halafu kukulazimisha ujishughulishe na kucheza dansi kwa kuvua nguo au vitendo vya biashara ya ngono (ukahaba).
- Kukuambia kwamba huna haki;
- Kukuambia kwamba hutaaminiwa au utafukuzwa nchini ukijaribu kutafuta msaada; au
- Kukuelekeza useme uongo kuhusu utambulisho wa mfanyabiashara haramu.

### Je, Utafukuzwa Nchini kama Ukiripoti Uonevu?

Kuna programu ya kulinda watu wanaoripoti uonevu. Usiogope kutafuta msaada hata kama una wasiwasi juu ya uhamiaji. Ushauriane na mwanasheria wa uhamiaji ambaye hamfanyii kazi mwajiri wako.



Kama unaamini wewe ni mhanga wa biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu au uhalifu mwingine mkubwa, ikiwa ni pamoja na ubakaji au mashambulio ya kingono, huenda ukastahili hadhi tofauti isiyo ya wahamiaji, kama vile "T" (kwa wahanga wa usafirishaji haramu) au hadhi ya "U" isiyo ya wahamiaji (kwa wahanga wa usafirishaji haramu au uhalifu mwingine mkubwa) au vinginevyo ukaruhusiwa kubaki kwa muda nchini Marekani. Aina hizi zisizo za wahamiaji zilianzishwa ili kulinda wahanga. Watu wengi nchini Marekani hawazijui sana hadhi za T au U zisizo za wahamiaji na labda utahitaji kuwaambia watu wanaokusaidia kuhusu hadhi hizo.

### Huduma Gani Zinapatikana kwa ajili ya Wahanga wa Biashara ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu?

- Wahanga wa Biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu nchini Marekani huenda wakastahili mafao, huduma na msaada wa uhamiaji chini ya programu za serikali kuu au majimbo. Mashirika mengi yanaweza kukusaidia kupata huduma hizi, zinazojumuisha huduma za matibabu/meno, huduma ya afya ya akili, makazi, msaada wa kisheria kwa ajili ya uhamiaji, na mahitaji mengine ya kisheria, msaada wa ajira, na mafao ya umma.

DOKEZO: Ni wazo zuri kuweka kumbukumbu ya maandishi ya muda wako wote unaofanya kazi. Pata daftari na andika siku zote na masaa yote ambayo ulifanya kazi, kiasi ambacho ulilipwa, tarehe ambazo ulipokea malipo, makato yoyote yaliyochukuliwa kutoka kwenye malipo yako, na sababu za makato hayo.

## SAMPULI YA ORODHA YA KUMBUKUMBU ZA KAZI KILA WIKI

| Mfanyakazi: | | Msimamizi: | |
|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Shughuli** | **Masaa** | **Malipo** |
| | | Kuingia:__________<br>Kutoka: __________<br>Jumla: __________ | |
| | | Kuingia:__________<br>Kutoka: __________<br>Jumla: __________ | |

# TEMBELEA TOVUTI HIZI KWA HABARI ZAIDI:

*(Tovuti zifuatazo ni za Kiingereza.)*

- Mchakato wa maombi ya viza na viza yako ya Kimarekani: *usvisas.state.gov.*
- Usafirishaji haramu wa binadamu: *www.state.gov/j/tip.*
- Programu ya viza ya J-1 ya mabadilishano: *j1visa.state.gov.*
- Usawa, na haki zako kuwa huru kutokana na ubaguzi kazini kwa sababu ya jadi yako, rangi, dini, jinsi (ikiwa ni pamoja na mimba), asili ya kitaifa, umri (miaka 40 au zaidi), ulemavu au habari za kijenetiki, na kuandikisha tuhuma ya ubaguzi: *www.eeoc.gov.*
- Haki zako za usalama kazini, au ukifikiria kazi yako si salama na unataka kuomba ukaguzi: *www.osha.gov.*
- Jinsi ya kupata mishahara unayomdai mwajiri wako: *ebapps.dol.gov/wow.*
- Haki zako za kulipwa malipo stahiki, ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuandikisha lalamiko kuhusu mshahara: *www.dol.gov/WHD/immigration.*
- Haki yako ya kutokabiliana na ubaguzi kwa sababu ya hadhi yako ya uraia na kuandikisha malalamiko dhidi ya ubaguzi: *www.justice.gov/crt/filing-charge.*
- Haki yako ya kujiunga na wafanyakazi wengine ili kuboresha mshahara wako au mazingira ya kazi, ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuandikisha tuhuma: *www.nlrb.gov.*
- Haki zako, wajibu, na misamaha ya bima ya afya: *localhelp.healthcare.gov.*

Kijitabu hiki kiliandaliwa kulingana na kifungu 202 cha Sheria ya mwaka 2008 ya William Wilberforce ya Kuidhinishwa Upya Ulinzi wa Wahanga wa Biashara Haramu, Sheria ya Umma 110-457.